

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA MIL. 863.2 KWA AJILI YA UJENZI WA
MIUNDOMBINU IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, Ndg. Kenneth K. Haule anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa, Halmashauri ya Mji Makambako imepokea fedha za ujenzi wa miundombinu idara ya elimu sekondari, kiasi cha shilingi 863,180,028 kwa mchanganuo ufuatao:-

1. Shilingi 583,180,028 ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Kata ya Mlowa, Mtaa wa Idofi kupitia Mpango wa Uboreshaji Elimu Kwa Shule za Sekondari (SEQUIP).
2. Shilingi 280,000,000 ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili na matundu 20 ya vyoo katika shule ya Sekondari ya Mbugani Kitandililo, kwa ajili ya maandalizi ya upanuzi wa shule kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha tano, ambapo gharama za ujenzi wa mabweni mawili ni shilingi 260,000,000 na matundu 20 ya vyoo ni shilingi 20,000,000.

Lina J. Sanga

Kaimu Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano ya Serikali

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

Julai 10, 2024